# UZALISHAJI BORA WA KONDOO WA NYAMA

## mtunze kondoo akutunze




**NA**

**EDITH E. NDEMANISHO**

# YALIYOMO

UTANGULIZI ........ 1

SURA YA KWANZA ........ 1

HALI YA SASA YA UFUGAJI WA KONDOO TANZANIA ........ 1

SURA YA PILI ........ 3

UZALISHAJI ........ 3

SURA YA TATU ........ 6

ULISHAJI ........ 6

SURA YA NNE ........ 9

AFYA YA KONDOO ........ 9

SURA YA TANO ........ 16

MABANDA ........ 16

SURA YA SITA ........ 18

UTUNZAJI KUMBUKUMBU ........ 18

# UTANGULIZI

Kitabu hiki, "Uzalishaji Bora wa Kondoo wa Nyama" kimetayarishwa na mtaalam na mfundishaji wa somo la mbuzi na kondoo kwenye Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (kwa zaidi ya miaka 35), Profesa Edith Ndemanisho. Lengo kubwa la kitabu hiki ni kuwaelimisha wafugaji wadogo wadogo wa kondoo juu ya ufugaji wa kisasa ili kuongeza pato na lishe kwa familia. Aidha, kimetayarishwa kwa kutumia lugha rahisi inayomwezesha mkulima kuelewa yaliyomo kwa urahisi. Nchini Tanzania kuna kondoo wanaokadiriwa kufikia milioni 6.0. Hadi sasa, kuna miradi michache sana ya utafiti na maendeleo ya uzalishaji wa wanyama hawa. Wafugaji wa kondoo hawajaelimishwa juu ya mbinu mbali mbali za uzalishaji. Kwa hiyo kuna matatizo mengi yanayoathiri shughuli za uzalishaji wa kondoo ikiwa ni pamoja na ulishaji bora, uzalishaji (breeding), mabanda, magonjwa na utunzaji kwa ujumla. Soko la kondoo ni kubwa hasa katika nchi za Uarabuni na huwa wanatafuta kondoo kwa wingi kutoka Tanzania. Ni vyema wafugaji wa kondoo wakachangamkia hili soko kwani majirani zetu Kenya huwa wanao kondoo bora ila idadi yake sio kubwa kama ya nchini Tanzania.

Kondoo wa nyama wanaweza kufugwa kwa gharama nafuu na kuishi katika mazingira magumu kama ya maradhi na ukame ikilinganishwa na ng'ombe. Kutokana na umbile lao dogo wanaweza kufugwa katika eneo dogo na pia wanaweza kuhudumiwa na familia yenye nguvu kazi na kipato kidogo. Uzao wao ni wa muda mfupi (anabeba mimba miezi mitano tu) unamwezesha mfugaji kupata kondoo wengi kwa kipindi kifupi. Wanyama hao hufugwa kwa ajili ya nyama, maziwa, ngozi, mbolea, sufu na mazao mengine kwa matumizi ya familia na kuongeza kipato.

Kitabu hiki kinaeleza mbinu mbali mbali juu ya utunzaji bora wa kondoo na kimegawanywa katika sura kuu sita ambazo ni *Hali ya sasa ya ufugaji wa kondoo Tanzania*, *uzalishaji*, *ulishaji*, *afya ya kondoo*, *mabanda* na *utunzaji kumbukumbu*.

## SURA YA KWANZA

## HALI YA SASA YA UFUGAJI WA KONDOO TANZANIA

### Kwa nini kondoo?

Kondoo ni wanyama wadogo ambao wakulima wenye kipato kidogo wanaweza kuwapata na kuwatunza kwa urahisi ukilinganisha na wanyama wakubwa kama ng'ombe. Kondoo wana faida zifuatazo:

- Wanachangia kipato cha mkulima kutokana na mauzo ya wanyama hai.
- Wanaweza kuzaa watoto wawili kwa mwaka hivyo huongezeka kwa haraka
- Wanahitaji sehemu ndogo ya malisho ikilinganishwa na wanyama wakubwa

- Samadi yao inaweza kutumika kuongeza uzalishaji wa mazao katika mashamba badala ya mbolea za viwandani.
- Mtaji mdogo unahitajika kuanza mradi wa uzalishaji wa kondoo
- Kondoo wana nafasi maalumu katika jamii. Kwa mfano, baadhi ya makabila hutumia kondoo katika shughuli za jamii kama mahari, vifo na sherehe za kimila
- Kondoo huchukua muda mfupi kufikia umri wa kuuzwa au kuchinjwa ikilinganishwa na ng'ombe
- Matumizi ya nyama ya kondoo anapochinjwa yanalingana na mahitaji ya familia bila ulazima wa kuhifadhi
- Hakuna pingamizi la kimila au kidini kuhusu ulaji wa nyama ya kondoo ikilinganishwa na nguruwe

**Je, hali halisi ya ufugaji wa kondoo Tanzania Ikoje?**

Tanzania ina kondoo zaidi ya milioni 6.0 ambao hupatikana karibu katika kila kijiji. Pamoja na idadi hii, kipato kutokana na wanyama hawa ni kidogo sana. Hii inatokana na utunzaji usio wa kitaalam. Kufuatia hali hii, uzalishaji upo katika viwango vya chini kama inavyoonyesha katika mifano ifuatayo hapa chini:

i) Wanyama hukua polepole (gramu 20-30 kwa siku)
ii) Vifo vya kondoo hutokea mara kwa mara. Wakati mwingine vifo vya watoto hufikia hadi asilimia 50 na vile vya kondoo wakubwa hufikia asilimia 30
iii) Kondoo huchelewa kupata mimba kwa mara ya kwanza. Hii inatokana hasa na lishe hafifu
iv) Kuna muda mrefu kati ya mzao mmoja hadi mwingine
v) Uzito wakati wa kuzaa au kuchinja huwa ni mdogo na huchukua muda mrefu kufikia uzito huo
vi) Ubora wa nyama ya kondoo hauridhishi kwa mahitaji ya soko

**Je ni mambo gani yanayochangia hali hii?**

i) Lishe hafifu
ii) Magonjwa
iii) Utunzaji mbaya
iv) Uduni wa wanyama
v) na utumiaji mbaya wa madume
vi) Kutokuwa na miongozo ya ufugaji bora wa kondoo

**Uzalishaji utakuwaje kama ufugaji bora ukizingatiwa?**

i) Ukuaji wa kondoo unaweza kuongezeka kutoka gramu 20 - 30 kwa siku hadi kufikia gramu 100 au zaidi kwa siku. Kwahiyo, wanaweza kuuzwa wakiwa na umri wa mwaka mmoja baada ya kuzaliwa
ii) Vifo vinaweza kupungua hadi kufikia asilimia 10, kiwango ambacho kinakubalika
iii) Mimba ya kwanza inaweza kushika kati ya umri wa miezi 8 hadi 12 kutoka miezi 18 - 24

iv) Kuongezeka kwa uzito wa kondoo wakati wa kuuza au kuchinja
v) Kupatikana kwa nyama inayokubalika zaidi na hivyo kujipatia soko la uhakika hasa kwenye mahoteli
vi) Kondoo wanaweza kuzaa mara tatu kwa miaka miwili

## SURA YA PILI

## UZALISHAJI

### Kuna aina ngapi za kondoo?

Kuna aina (breeds) nyingi sana za kondoo duniani na Afrika Mashariki. Aina za kondoo hutofautiana sana kwa ukubwa, umbile na wingi na urefu wa manyoya. Pia hutofautiana katika ukubwa na maumbile ya pembe zao, mikia yao na masikio. Licha ya tofauti hizi nyingi, urefu na unene wa mikia yao vimekuwa vigezo muhimu katika kuelezea aina za kondoo. Kuna kondoo wenye mikia;

- Mirefu miembamba
- Mifupi miembamba
- Mirefu minene
- Mifupi minene
- Yenye mafuta mengi

### Kuna aina ngapi muhimu za kondoo Tanzania?

Nchini Tanzania kuna aina kuu tatu za kondoo zinazotambulika

a) Maasai

Ni aina ya kondoo wanaofugwa na kabila la Kimaasai na wameenea sehemu nyingi za Tanzania na hata Kenya. Kondoo hawa wana rangi nyekundu au wekundu na mabaka meupe. Hawa ni wa nyama wenye mafuta mengi sana kwenye mikia yao ambayo ni mifupi.

- Kondoo waliokomaa wana uzito huu:- madume kilo 25 hadi 35; majike kilo 25 hadi 28. Madume yaliyohasiwa na kulishwa vizuri huweza kufika kilo 50
- Ni mara chache mno kuona kondoo hawa wakizaa watoto mapacha
- Wanastahimili sana magonjwa ya kwato na minyoo
- Kondoo hawa hufugwa haswa kwa ajili ya nyama yao nzuri na mafuta

b) Kondoo wa Kigogo (**Gogo type**)

- Ni kondoo wanaofugwa sana na kabila la Wagogo
- Ni wadogo kwa umbile na wana rangi ya udongo
- Wana mikia mirefu na masikio yao ni madogo na wakati mwingine huwa ni ‘vibutu’ (ni kama masikio yaliyokatwa karibu na kichwa)

c) Blackhead Persian (**BHP**) au kondoo wa Somali
   - Hii ni aina ya kondoo inayotoka kaskazini mashariki mwa Afrika (*Somali land*) ndiyo sababu ya kuitwa kondoo wa Somali. Kondoo hawa hupatikana pia Afrika ya kusini ambako wametumika sana kuzalisha aina nyingine za kondoo



**A. Kondoo wa Masai**



**B. Kondoo wa Somali**

   - Ni kondoo wenye shingo na vichwa vyeusi ila sehemu nyingine za mwili na miguu zina manyoya mengi meupe. Mikia yao ni mifupi yenye mafuta mengi hadi kufikia zaidi ya kilo 10. Hutunzwa sana kwa ajili ya nyama.
   - Kondoo waliokomaa wana uzito mkubwa zaidi ya kondoo wa Maasai. Wanayo miguu mirefu na miembamba na kwato zao ni rahisi kupata ugonjwa hasa katika sehemu zenye unyevunyevu. Ni kondoo wanoaweza kuishi kwenye maeneo yenye ukame. Wana masikio madogo na hawana pembe kabisa.

**Kumbuka: Kondoo wa BHP ndio wanaopendekezwa katika kuzalisha machotara. Hii ni kwa sababu machotara hao wanachukua muda mfupi kufikia uzito wa kuuza.**

**Upandishaji**

**Je, utawapandisha kondoo majike wakati gani?**

- Majike wadogo huanza kutoa mayai katika tumbo la uzazi wakiwa na umri wa miezi kati ya 6 na 8. Hata hivyo, inapendekezwa asipandishwe wakati huu.
- Inashauriwa apandishwe kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miezi 8 hadi 12 kutegemeana na ukuaji wake na umbile lake. Umbile lake linatakiwa liwe kubwa kumuwezesha kubeba mimba vizuri na kuzaa bila matatizo.
- Mimba ya kondoo huchukua siku 150 au miezi 5. Baada ya kuzaa, kondoo jike huja kwenye joto wiki 2 hadi 3 zifuatazo, lakini kuna kondoo wengine hawapati joto mwezi mmoja mpaka miwili baada ya kuzaa kwa sababu ya kunyonyesha.
- Joto ni hali ya mnyama (kondoo jike) kuhitaji dume kumpanda apate mimba.
- Joto la kondoo hurudia kila baada ya siku 15 hadi 19 na muda wa joto ni saa 18 mpaka 24. Ni muhimu kumpandisha kondoo jike mara anapoonekana yupo kwenye joto. Inabidi

kutunza kumbukumbu za upandishaji, ili kuweza kufuatilia joto la kondoo kwa nia ya kuelewa kama amepata mimba au la. Kondoo akipandishwa miezi 3-4 baada ya kuzaa anaweza kuzaa mara 3 katika miaka 2.

**Madume**

**Ni lini madume ya kondoo yaanze kutumika?**

- Madume madogo huanza kutoa mbegu yakiwa na umri wa miezi 5 hadi 10. Lakini madume yaliyochaguliwa kwa jili ya uzazi yaanze kutumika kupanda **majike machache** yakifikia umri wa miezi kati ya 12 na 18. Baada ya umri wa miaka miwili, dume mmoja linaweza kukaa na majike kati ya 20 hadi 30 muda wote.
- Madume bora tu yatumike katika uzalishaji.

**Je uchaguzi wa dume bora unazingatia sifa zipi?**

- Awe ametokana na wazazi wenye sifa nzuri za ukuaji, kuzaana na ubora wa maumbile.
- Ukuaji uwe mzuri sana ukilinganisha na madume mengine kundini.
- Awe na umbile kubwa na kujaza misuli sawasawa.
- Asiyeugua mara kwa mara.
- Awe na umbile la kiume na sehemu zake za uzazi ziwe sawasawa

**Kuzaliana kiukoo**

**Kuzaliana kiukoo ni nini na madhara yake ni nini?**

- Katika jamii zote za wanyama, kuzaliana kiukoo hakuruhusiwi kabisa. Hii ina maana kwamba si vyema kumpandisha dume kwa mama yake, kondoo jike kwa baba yake, au hata kuwapandisha watoto wa baba na mama mmoja. Huko ni kuzaliana kiukoo.
- Matokeo ya kuzaliana kiukoo ni kuzaliwa kondoo vilema au wanaokufa wakiwa wachanga. Aidha, watoto hao huzaliwa wakiwa wadhaifu na hukua kwa matatizo sana.

**Utazuiaje kondoo wako kuzaliana kiukoo?**

Ili kuzuia kondoo wako kuzaliana kiukoo, zingatia yafuatayo:-

- Wahasi au wauze madume wote waliozaliwa shambani mara baada ya kuachishwa kunyonya.
- Kama unaweza kuwa mwangalifu na makini, tunza kumbukumbu za upandishaji kila mwaka na hatimaye ufuatilie uhusiano wa kondoo wako ili usipandishe kondoo ambao wana uhusiano wa karibu.

**Zingatia: Madume yatumikayo kupanda yasikae katika kundi la majike yako kwa zaidi ya mwaka mmoja na inashauriwa wafugaji wabadilishane madume baada ya muda huo.**

# SURA YA TATU

## ULISHAJI

**Kondoo hupenda kula nini?**

- Aina mbalimbali za majani; wanapochungwa huanza na yale laini. Mchanganyiko wa majani wanaokula kondoo huwawezesha kupata viinilishe mbalimbali vya vyakula, kama vile protini, wanga (nguvu), madini na vitamin. Hii inawafanya wawe na afya nzuri na kukua kwa haraka.
- Matawi ya miti hasa mikunde kama vile lukina, mlonge, mfifi na migunga. Kondoo hawapendi kusimama na kula matawi ya miti kama wafanyavyo mbuzi. Kwa hiyo, ni vyema matawi haya yakatwekatwe au yatundikwe karibu nao.



C. Lukina



D. Mlonge

- Mabua ya mahindi na mazao mengine kama nyasi za mpunga, maharage au ngano. Mabua haya yanaweza kuboreshwa kwa kutumia mbolea ya urea, kinyesi cha kuku na majivu.
- Mabaki ya jikoni kama majani ya mboga (kabichi, mchicha na matembele) na maganda ya matunda mbalimbali
- Ngugu inaliwa sana na kondoo, ila ikatwe vipande vidogo vidogo kwa panga au mashine na kuwekwa kwenye vyombo maalum (*feed troughs*) kuzuia umwagikaji. Vyombo hivi vya chakula visafishwe kuzuia wadudu wanaoleta magonjwa ya kuharisha.

**Ulishaji wa kondoo**

Kuna aina ngapi za ulishaji wa kondoo?

Hapa Tanzania na mahali pengine katika nchi za joto kuna aina mbili kuu za ulishaji

i. Kuchunga
ii. Kuwalisha nyumbani

**Kuchunga:**

Huku ni kuwapeleka kondoo machungani wazunguke wakila chochote wanachofanikiwa kukifikia au kuwafunga kwa kamba hapa na pale porini (hasa kama ni kundi dogo). Inashauriwa kuwahamishia wanyama kwenye sehemu mpya zenye majani mabichi mara kwa mara ili kuwawezesha wapate viinilishe na virutubisho vya kutosha.

- Huu ni mfumo wa ufugaji wa kondoo wa nyama unaotegemewa sana Tanzania. Hii ni kwa sababu, ukiwa na kondoo wengine (50 au zaidi), ni vigumu kuwalisha ndani ya banda kwa muda wote.
- Muda wa kondoo kuchungwa usipungue saa 8 kwa siku ili washibe na kupata viinilishe na virutubisho vya kutosha wanavyostahili kwa afya zao.
- Eneo la kuchungia liwiane na wingi wa wanyama ili wapate chakula cha kutosha na kuzuia uwezekano wa milipuko ya magonjwa, na mmomonyoko wa udongo.
- Kondoo wasilishiwe sehemu moja kila siku, bali wazunguke maeneo mbalimbali. Mzunguko huo pia hutoa nafasi kwa malisho kuota upya sehemu moja wakati kondoo wamehamishiwa sehemu nyingine.

**Faida za kuchunga**

- Gharama za ulishaji ni ndogo kwa sababu mnyama anajitafutia anachotaka
- Wanyama wanapata hewa ya kutosha, afya nzuri na kuchangamka zaidi kulingana na hali ya hewa hasa kama kuna jua la wastani na hakuna mvua.

**Kuwalisha nyumbani**

Kondoo huachwa kwenye banda, boma au kufungiwa kando ya banda. Chakula kama majani huletwa kwa mnyama. Kwa kawaida mfumo huu wa ufugaji unafaa pale tu mfugaji akiwa na wanyama wachache na hana maeneo makubwa ya kuchungia.

**Faida za kulisha nyumbani**

- Kondoo hawahitaji eneo kubwa la malisho
- Wanaweza kutumia mazao na mabaki mengi ya shamba kama vile majani ya migomba, mahindi, mabaki ya maharage na hata matawi ya miti mbalimbali
- Inapunguza muda wa kuchunga. Wanaweza kuzungushiwa boma ili wapate mazoezi na sehemu ya kupata jua (Vitamini D)
- Ni rahisi kupanga na kumudu uzazi
- Hupunguza kondoo kuharibu mazao kwa majirani na kuepuka ugomvi nao
- Inarahisisha ukusanyaji wa mbolea
- Huzuia maambukizi ya magonjwa, ila kondoo wasisongamane kwenye banda

Hata hivyo, katika hali halisi ya wafugaji, si rahisi kuwalisha kondoo nyumbani. Kwa kawaida kondoo wa nyama ni wa kuchungwa.

**Ni mambo gani ya kuzingatia katika ulishaji wa kondoo?**

- Lisha chakula kisafi na majani yasiyo na unyevunyevu
- Maji na vyombo view visafi
- Kondoo wapate mchanganyiko wa vyakula vyote yaani majani ya asili ya nyasi, mikunde na madini.
- Kondoo wanaolishwa ndani wanaweza kuwekewa vitita vya majani wakati wote.
- Tumia mabaki ya mazao kama mabua ya mahindi, mtama na mabaki ya maharage, ngano, n.k. Ubora wa mabaki haya unaweza kuongezeka kama ukichanganya na mollasis, urea kutegemea upatikanaji wake.
- Miezi michache kabla ya kuuza kondoo, mabaki haya na mashudu yanaweza kutumika kumnenepesha kondoo iliapate bei nzuri wakati wa kuuza.
- Kondoo wa marika yote wapewe jiwe la kulamba (madini).
- Aina ya mikunde laini isilishwe kwa wingi kwa vile kondoo huweza kuvimbiwa (bloat).
- Chakula kisiwekwe sakafuni. Hii ni kwa sababu kinaweza kuharibika na kuchafuliwa na vijidudu, kinyesi na mkojo.
- Ulishaji wa kondoo kwenye mashamba ya mahindi, mtama, n.k. baada ya mavuno husaidia sana hasa wakati wa kiangazi. Vile vile rutuba ya udongo huongezeka kutokana na kinyesi cha kondoo.
- Utumiaji mzuri wa miti ya malisho huongeza lishe bora kwa kondoo. Miti hii ni kama lukina, Mlonge, Sesbania, Mfifi, Migunga na Kaliandra. Inaweza ikaoteshwa mipakani mwa shamba la mazao au hata ndani ya shamba. Ikiwezekana kondoo wapewe majani ya miti hiyo baada ya kutoka machungani.
- Miti ya asili kama migunga, mikwaju, n.k. isikatwe ovyo ovyo sehemu wanakochungia kondoo. Matunda na majani ya miti kama hiyo ikichanganywa na malisho huboresha chakula kwa kuongeza protini. Kwa sababu kondoo hawajazoea kutumia majani ya juu kama mbuzi mchungaji awadondoshee matunda na majani ya miti hiyo.
- Majani ya asili yanaweza kuboreshwa kwa kusia mbegu za mikunde katika mbuga hizo za malisho.
- Kutegemeana na hali ya uchumi, kondoo huweza kupewa vyakula vya ziada kama pumba, mashudu na mchanganyiko wa madini.

# SURA YA NNE

## AFYA YA KONDOO

### Utangulizi

Kondoo wakishambuliwa na magonjwa huwa wanaonyesha dalili zinazomuashiria mfugaji kuwa kondoo wanaumwa. Wafugaji wanashauriwa kutambua mapema dalili za mwanzoni kabisa. Dalili kubwa ni kujitokeza kwa hali isiyokuwa ya kawaida kwa kondoo. Hivyo basi, ni muhimu kwa mfugaji awe na ufahamu mzuri na kondoo wake na awe anawafuatilia kwa karibu ili aweze kugundua mabadiliko yoyote yasiyo ya kawaida yatakayotokea. Mara tu ugonjwa wowote utakaposhukiwa kujitokeza, mfugaji anapaswa kutoa taarifa kwa mganga wa mifugo mapema ili apatiwe huduma.

Ni muhimu kuelewa hali ya afya ya kawaida kwanza ili baadaye uweze kutambua hali isiyo ya kawaida ambayo ni ya ugonjwa.

### Je ni madhara gani yatokanayo na kondoo wasio na afya nzuri?

Kondoo wasio na afya nzuri humletea mfugaji hasara za kiuchumi kutokana na;

- Vifo
- Kupungua uzito
- Kukua polepole na kuchelewa kufikia uzito wa kuuza
- Gharama kubwa za matibabu
- Baadhi ya magonjwa ya kondoo huathiri binadamu (*Zoonotic*)
- Kutupa mimba

### Kondoo mwenye afya anaonekanaje?

- Amechangamka na kichwa chake huwa juu.
- Macho yake ni maangavu. Pia huzungusha masikio pindi inapotokea sauti.
- Mwili wake umejaa vizuri (hajakonda)
- Manyoya yanang'ara na yanalala vizuri juu ya ngozi yake.
- Anafuatana na wenzake kwenye kundi.
- Anakula vizuri kisha baadaye anacheua na kutafuna tena (*chewing the cud*)
- Anatoa kinyesi kawaida
- Vipimo vya mwili ni vya kawaida (joto la mwili $38.5^0$C hadi $40^0$C na mapigo ya moyo ni 70-80 kwa dakika, na anavuta pumzi mara 12-20 kwa dakika)
- Rangi ya ngozi ya ndani ya jicho ni pinki

**Dalili gani zinazoonyeshwa na kondoo wasio na afya nzuri?**

- Kondoo kujitenga na wenzake
- Kuachia kichwa kiende chini
- Kupunguza hamu ya kula na hata kutokula kabisa
- Kutokuwa mchangamfu (kuzubaa)
- Kusisimuka manyoya, kuonekana hana nguvu, kuchoka na inzi hutua mwilini mwake
- Kuishiwa nguvu na kushindwa kusimama na kutembea
- Kubadilika kwa vipimo vya joto, mapigo ya moyo na kuvuta pumzi
- Kuharisha au kutoa kinyesi kigumu kupita kiasi
- Kupumua kwa shida

**Kumbuka: NI RAHISI KUZUIA KULIKO KUTIBU**

Kuzuia magonjwa hutumia fedha kidogo tu kulinganisha na gharama za kutibu ambazo ni pamoja na madawa ya bei kubwa, hasara kutokana na vifo, na kushuka kwa uzalishaji. Kwa hiyo hapa tumeorodhesha baadhi ya magonjwa muhimu ya kondoo hapa Tanzania.

**Kuna makundi mangapi ya magonjwa ya kondoo?**

Kondoo, kama walivyo wanyama wengine wafugwao, huweza kushambuliwa na magonjwa mengi. Magonjwa haya yametapakaa na kuenea mikoa yote Tanzania na kuathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa kondoo. Magonjwa ya kondoo yanaweza kupangwa katika makundi makuu yafuatayo:

a) Magonjwa yanayoambukizwa kwa haraka na yenye kutia hasara kubwa (magonjwa ya mlipuko) kama vile Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever*, RFV), ugonjwa wa miguu na midomo (FMD)
b) Magonjwa yasiyo ya mlipuko lakini yanayoua kondoo kwa wingi kwa mfano Kimeta
c) Magonjwa yanayoifanya Tanzania kutokubalika kuuza mifugo yake na mazao ya mifugo katika soko la kimataifa, k.m. FMD
d) Magonjwa yanayoambukiza wanadamu (Zoonoses), k.m. Kimeta, ndui (*Orf*), Homa ya bonde la Ufa (Rift Valley Fever - RFV)

**Minyoo**

**Minyoo ni nini na inapatikana wapi?**

Minyoo ni viumbe hai wenye ukubwa mbalimbali ambao wanaishi kwa kutegemea wanyama wengine. Minyoo wanapatikana katika tumbo, utumbo, maini na mapafu ya wanyama.

**Dalili za kondoo wenye minyoo ni zipi?**

Kondoo anaweza kuonyesha baadhi ya dalili zifuatazo;

- Vifo vya ghafla hasa kwa watoto wa kondoo
- Hamu ya chakula inashuka, wanakuwa hawana nguvu na tumbo kuvimba
- Manyoya yaliyosimama na yasiyopendeza
- Kupungukiwa damu (Macho huwa meupe badala ya rangi ya pinki)
- Kuharisha
- Kondoo hupunguza ukuaji na hukonda
- Kupata uvimbe kwenye taya la chini
- Kuzuia usagaji wa chakula tumboni na wakati mwingine kuziba utumbo
- Kondoo wakubwa huwa dhaifu na hatimaye hufa



**E. Kondoo mwenye uvimbe taya la chini**



**F. Kondoo mwenye macho meupe**

**Utatibu na kuzuiaje minyoo kwenye kondoo?**

- Tumia dawa ya kuua minyoo mfano; Albendazole (ya kunywesha/maji au vidonge), Levamisole (yakuchoma chini ya ngozi), Ivomectin (yakuchoma chini ya ngozi)
- Banda liwe safi pia nyunyizia dawa ya kuua wadudu
- Tumia dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu hasa wakati wa masika.

**Muhimu**: Tafuta ushauri wa mtaalam kuhusu matumizi ya madawa

**Ugonjwa wa kuharisha damu (*coccidiosis*)**

**Ugonjwa wa kuharisha damu unasababishwa na nini?**

Ugonjwa wa kuharisha damu unaweza kusababishwa na vitu vingi, lakini mara nyingi huletwa na vimelea vinavyoitwa *coccidia*

- Kondoo wadogo huathirika zaidi kutokana na chakula na maji yenye vimelea
- Vimelea hutoka kwenye kinyesi cha kondoo wakubwa na kuchafua mazingira

**Dalili za ugonjwa wa kuharisha damu ni nini?**

- Kushindwa kula, kukosa nguvu na kukonda
- Kuharisha damu na kujikamua wakati wa kuharisha
- Vifo vya kondoo wadogo

**Je unawezaje kuzuia na kutibu ugonjwa wa kuharisha damu?**

- Kutumia sulphadimidine na amprolium
- Tenganisha wagonjwa na kuwatibu
- Weka kondoo sehemu safi na kavu
- Hakikisha kinyesi hakichafui maji na chakula
- Punguza msongamano wa kondoo katika banda

**Ugonjwa wa moyo kujaa maji (*Heartwater*)**

**Ugonjwa wa moyo kujaa maji ni nini?**

- Ugonjwa huu unaodhuru ng'ombe, mbuzi na kondoo unaletwa na vimelea vinavyosambazwa na kupe.

**Dalili za ugonjwa wa moyo kujaa maji ni zipi?**

- Homa kali na kupoteza hamu ya kula
- Dalili za kichaa kama kupoteza utaratibu wa hatua, kutembea kwenye mduara na kusaga meno
- Kuanguka, kutetemeka, kupiga mateke na halafu kufa
- Maji mengi kwenye moyo, kifua na tumboni mwa mzoga

**Je utazuiaje ugonjwa wa moyo kujaa maji?**

- Tumia dawa ya josho kuuwa kupe
- Tumia dawa ya tetracycline kutibu wagonjwa

**Kuoza kwato (*Foot rot*)**

**Ugonjwa wa kuoza kwato ni nini?**

- Ugonjwa huu wa kuoza kwato unasababishwa na bakteria ambao huzaliana kwenye kwato

- Maambukizi hutokea kwenye matope hasa kipindi cha mvua

**Dalili za kuoza kwato ni zipi?**

- Kuvimba miguu na kwato kuwa na joto
- Vidonda kwenye kwato vinavyosababisha maumivu makali
- Kuchechemea

**Je, unazuiaje na kutibu ugonjwa wa kuoza kwato?**

- Weka kondoo sehemu kavu
- Kata kwato ndefu
- Tibu vidonda kwa kuviosha na kuweka dawa
- Tumia dawa ya sindano *sulphadimidine* kutibu

**Ugonjwa wa kondoo wa Nairobi (Nairobi sheep disease)**

**Ugonjwa wa kondoo wa Nairobi ni nini?**

Ni ugonjwa wa kondoo na mbuzi unaosababishwa na virusi vienezwavyo na kupe

**Dalili za ugonjwa wa kondoo wa Nairobi ni zipi?**

- Homa kali
- Kutokwa na makamasi yaliyochanganyika na damu au usaha
- Kuharisha damu na kuambatana na harufu mbaya na kujikamua sana akiharisha
- Kutupa mimba
- Vifo kwa wingi

**Je, unazuiaje ugonjwa wa kondoo wa Nairobi?**

- Ogesha ili kuua kupe

**Ugonjwa wa ulimi wa bluu (Blue tongue)**

**Ugonjwa wa ulimi wa bluu ni nini?**

- Ni ugonjwa wa kondoo, ng'ombe na mbuzi unaosababishwa na virusi vinavyoenezwa na wadudu wanaong'ata wanyama (*Culicoides spp*)

**Dalili za ugonjwa wa ulimi wa bluu ni zipi?**

- Homa kali
- Uvimbe wa taya
- Kutoka damu puani, mdomoni na kope za macho
- Ulimi kuwa mwekundu na baadaye kuvimba na kuwa wa bluu halafu kuning'inia nje ya mdomo
- Vidonda puani, mdomoni, mashavuni na kwenye miguu

- Makamasi mazito yanayoweza kuziba pua
- Kuzaa watoto vilema

**Je, unazuiaje ugonjwa wa ulimi wa bluu?**

- Njia moja kuu ni kuchanja kondoo dhidi ya huu ugonjwa

**Je, unatibiaje ugonjwa wa ulimi wa bluu?**

- Kondoo wenye ugonjwa wa ulimi wa bluu hutibiwa kwa kuchomwa antibiotic.
- Pia kutoa ripoti kwa daktari wa mifugo.

**Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever*)**

**Ugonjwa wa homa ya Bonde la Ufa ni nini?**

- Ni ugonjwa wa mlipuko unaosababishwa na virusi na kusambazwa na mbu
- Unaathiri kondoo, mbuzi, ng'ombe na binadamu.

**Dalili za homa ya Bonde la Ufa ni zipi?**

- Homa
- Kutokwa makamasi
- Kutupa mimba
- Vifo vya kondoo wadogo

**Je, unazuiaje na kutibu ugonjwa wa homa ya bonde la ufa?**

- Chanja kondoo
- Kuzuia mazalia ya mbu

**Ugonjwa wa Miguu na Midomo (*Foot and Mouth Disease* - FMD)**

**Ugonjwa wa Miguu na Midomo ni nini?**

- Ni ugonjwa wa mlipuko unaoathiri kondoo, mbuzi, nguruwe, ng'ombe na wanyama pori unaosababishwa na virusi.

**Dalili za ugonjwa wa miguu na midomo ni zipi?**

- Homa kali
- Kutokula
- Vivimbe au vidonda kwenye ulimi, fizi, midomo, puani, miguuni, kwenye chuchu na kiwele
- Kuchechemea na kutokwa mate mengi mdomoni

**Je utazuiaje ugonjwa wa miguu na midomo?**

- Karantini ya kuzuia usafirishaji wa mifugo na mazao ya mifugo

- Chanja mifugo kila mwaka au kila mlipuko utokeapo

**Magonjwa ya mapafu (*Pneumonia*)**

**Ugonjwa wa mapafu ni nini?**

- Ni ugonjwa unaoathiri mapafu ya kondoo unaosababishwa na vimelea vya aina nyingi kama virusi, bakteria, *mycoplasma, chlamydia* na minyoo ya mapafu

**Dalili ya ugonjwa wa mapafu ni zipi?**

- Kukohoa
- Kutokwa makamasi
- Kupumua kwa shida
- Vifo

**Utazuiaje ugonjwa wa mapafu?**

- Weka kondoo sehemu safi na kavu
- Epuka msongamano wa kondoo

**Kimeta (Anthrax)**

**Ugonjwa wa kimeta ni nini?**

- Ni ugonjwa hatari unaoathiri wanyama wote wenye damu moto pamoja na binadamu unaosababishwa na bakteria

**Dalili za kimeta ni zipi?**

- Homa kali
- Vifo vya ghafla bila dalili nyingine
- Kupumua kwa shida
- Kutetemeka na kifafa
- Kusitisha kucheua
- Kutupa mimba
- Kutoka damu nyeusi isiyoganda kwenye matundu ya mwili
- Mzoga wa kimeta hauonyeshi kugangamala misuli

**Utazuiaje ugonjwa wa kimeta?**

- Chanja mifugo
- Karantini ya usafirishaji wa mifugo
- Mzoga wa kimeta umwagiwe chokaa na ufukiwe au uchomwe moto bila kupasuliwa


Mfugaji anapoona dalili za ugonjwa huu kwenye kondoo anashauriwa kumwona daktari wa mifugo ili aweze kuutambua ugonjwa na kutibu. Aidha, mfugaji atapewa ushauri wa njia sahihi za kukinga wanyama wake wasiambukizwe na kuugua tena hapo baadaye.

# SURA YA TANO

## MABANDA

### Hali halisi ya mabanda ya kondoo Tanzania

Kondoo huchungwa porini pamoja na ng'ombe na mbuzi. Wakirudi jioni huwa wanawekwa kwenye boma lililozungushiwa aidha kwa miiba, ukuta wa miti au mabanzi. Wakati mwingine huishi nyumba moja na wanaadamu. Kwenye maboma, kondoo hunyeshewa mvua na mara nyingi hukaa kwenye mazingira ya matope. Matatizo mengi yanaambatana na ufugaji wa namna hii, ikiwa ni pamoja na kuingiliwa na wanyama wakali, uchafuzi wa mazingira, maambukizi ya magonjwa hata kwa wanaadamu.



G. **Banda la chini la kondoo**




**H. Bandaa la juu la kondoo**

### Je, ni muhimu kujenga banda la kondoo?

Umuhimu mkubwa wa banda kwa wanyama hawa, kama ilivyo kwa wanyama wengine wowote ni katika kuwapa kivuli, kuwakinga na mvua, wanyama wa porini na kuzuia wezi. Katika ufugaji wa kisasa wa kondoo, banda linajengwa ili kukidhi mambo mawili:

a) Kuyaweka mazingira ya kondoo katika ubora zaidi
b) Kurahisisha huduma kwa kondoo (kulisha, kutibu, kuchanja n.k.)

Kondoo huhitaji mazingira ambayo

a) Sio baridi wala joto sana
b) Yasiyo na unyevunyevu wala matope
c) Yasiyo na wadudu kama vile inzi, viroboto, utitiri, n.k.
d) Yenye hewa safi, mwanga na nafasi ya kutosha

**Aina gani ya banda hufaa kwa ajili ya kondoo?**

Aina ya banda la kondoo hutegemea mfumo wa ufugaji pamoja na idadi ya kondoo wanaofugwa:

a) Banda la gharama huweza kuhitajika pale tu ambapo uzalishaji ni wa kiwango cha juu. Ni lazima kulinganisha kipato na gharama za banda.
b) Katika ufugaji wa kuwachunga kondoo katika nyanda za malisho (porini), banda la kawaida linatosha. Banda kama hilo linaweza kuwa na paa, au likawa la kuweka kondoo sehemu moja wakati wa usiku.

**Ni vifaa gani vitumike kujenga banda la kondoo?**

Inasisitizwa kwamba vifaa vya kujengea banda la kondoo viwe ni vile vinavyokidhi haja bila kuwa na gharama sana. Pia viwe ni vile vinavyopatikana kwa urahisi katika eneo la mfugaji:

**i. Paa**

- Katika nchi za joto kama Tanzania, paa ni muhimu katika nyumba ya kondoo kwani humsitiri kondoo kutokana na jua kali na mvua
- Ni vizuri paa likawa na mteremko wa kutosha ili liweze kuhimili upepo mkali na kupunguza uwezekano wa kuvuja
- Vifaa vitumikavyo kuezekea banda ni nyasi, makuti ya minazi, makuti ya michikichi, majani makavu ya migomba na bati

**ii. Kuta**

Kuta za banda la kondoo mara nyingi hupashwa kutoa fursa ya hewa kuzunguka nje na ndani ya banda. Hali hiyo ni muhimu katika,

- Kuondoa joto na kupunguza unyevunyevu
- Kuondoa hewa chafu toka bandani na kuingiza hewa safi
- Wakati mwingine ukuta huweza kuzibwa sehemu fulani kulingana na kinachopashwa kuzuiwa kisiwafikie kondoo kama vile upepo mkali. Palipo na wasiwasi wa wanyama wakali na/au wizi, ukuta sharti uwe imara.

Vifaa vinavyoweza kutumika kwenye kuta ni nguzo, fito, mabanzi, udongo, bati, waya meshi na matofali

**iii. Sakafu**

Kinachotakiwa katika utengenezaji wa banda la kondoo ni sakafu kuwa kavu wakati wote. Ingawa ni vizuri kuwa na sakafu iliyoinuliwa kufanikisha suala la ukavu, siyo lazima sana kuinua sakafu kwani sakafu ya chini inaweza kuwa na mteremko unaotosha kutiririsha maji na mkojo kutoka kwenye banda

Vifaa vinavyoweza kutumika kwenye matengenezo ya sakafu ya chini ni mbao, mianzi, mabanzi, fito na wayameshi.

## SURA YA SITA

## UTUNZAJI KUMBUKUMBU

**Je, kumbukumbu ni nini?**
Kama ilivyo vitega uchumi vingine, utunzaji wa kumbukumbu ni muhimu sana ili kujua ufanisi wake hasa hasa mapato na matumizi. Kumbukumbu husaidia kufuatilia maendeleo ya kila kondoo, hutuwezesha kuelewa kondoo wazuri na wabaya. Pia kumbukumbu hutumika kutathimini magonjwa na matatizo mengine yaliyopo katika kundi lako la kondoo. Waghani watakushauri vizuri zaidi wakiziona kumbukumbu zako.

**Utunzaji wa kumbukumbu za mifugo**
Kuweka kumbukumbu za mifugo ni muhimu katika uzalishaji kwa ajili ya kutambua kosaafu, gharama za utunzaji na faida. Pia, humsadia mfugaji kufanya maamuzi katika uendelezaji wa ufugaji wake. Mtalaam wa mifugo pia anaweza kutumia kumbukumbu hizi ili kumsaidia mfugaji kuboresha ufugaji wake.

**Kuna aina ngapi za kumbukumbu?**

- Kuna aina nyingi za kumbukumbu kutegemeana na mfugaji anataka kufuatilia kitu gani kwa mfano mapato na matumizi, maendeleo ya kila kondoo. Jinsi ya kuandika kumbukumbu hutofautiana pia. Wengine hufuata majedwali maalum yaliyoandaliwa na wataalam wa mifugo na wengine huandika wapendavyo wenyewe. Hapa tunapendekeza aina chache za kumbukumbu unazoweza kuandika:

i) Kumbukumbu za uzazi: Onyesha kondoo gani amezaa, lini, jinsia ya mtoto, baba wa mtoto, aina (breed) na ikiwezekana uzito wa kuzaliwa

**JEDWADWALI NA. 1**

| **Tarehe ya kuzaliwa** | **Na. ya kondoo** | **Jinsia** | **Aina** | **Namba ya** | | **Uzito wa kuzaliwa (kilo)** | **Mengineyo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Baba | Mama | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

ii) Kumbukumbu za chanjo na matibabu: Andika tarehe ya tukio, namba ya kondoo, aina ya chanjo/ugonjwa aliokuwa nao, aina ya dawa iliyotumika na gharama za matibabu

iii) Kumbukumbu za ukuaji: Kama kondoo wanapimwa uzito mara kwa mara, ni muhimu kuweka kumbukumbu za huo uzito. Inafaa kuandika tarehe ya kupima, namba ya kondoo na uzito wake. Ongezeko la uzito linaonekana vizuri zaidi ikiwa, uzito wa kondoo mmoja utapangwa katika mstari mmoja

**JEDWALI NA. 2**

| Na. ya kondoo/jina | Tarehe ya kupima uzito (kilo) | | | | | | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.11.2020 | 15.3.2020 | | | | | |
| Ishia/157 | 10.5 | 14.6 | | | | | |

iv) Kumbukumbu nyinginezo: Kama tulivyosema hapo juu, unaweza kuandika mambo mengine yanaohusu kondoo wako kwa mfano, kuachisha kunyonya, kuuza kondoo, kuhasi kondoo, manunuzi mbalimbali (dawa, vifaa, vyakula). Ni muhimu kuandika tarehe ya tukio

**Utawezaje kuwatofautisha kondoo kabla ya kutunza kumbukumbu?**

Ili mfugaji aweze kutunza kumbukumbu za kila kondoo, inabidi aweze kuwatofautisha kwa kuwapa vitambulisho. Njia zifuatazo zinaweza kutumika: -

a. Kwa kuwavalisha kamba zenye vibao vyenye namba shingoni
b. Kuwapa majina, kwa mfano Sabasaba, Ufunuo na kadhalika
c. Kuwaweka hereni (ear-tag) za plastiki au za chuma kwenye masikio